# PRE-MOCK

*Kenya Certificate of Secondary Education (K.C.S.E)*

**KISWAHILI 102 / 2**

**MUDA: SAA 2 ½**

**(Ufahamu, Ufupisho, Matumizi ya Lugha, Isimu-Jamii)**
**Jibu maswali yote;**

**JINA..........................................................................................TAREHE.................................**

**NAMBARI YAKO...................................................................DARASA...............................**

**Majibu yote yaandikwe katika nafasi zilizoachwa katika kijitabu hiki cha maswali. Karatasi hii ina kurasa 9. Watahiniwa ni lazima waangalie kama kurasa zote za karatasi hii zimepigwa chapa sawasawa na kuwa maswali yote yamo.**

**KWA MATUMIZI YA MTAHINI PEKEE.**

| Swali | Upeo | Alama |
|---|---|---|
| 1 | 15 | |
| 2 | 15 | |
| 3 | 40 | |
| 4 | 10 | |
| Jumla | 80 | |

for free past papers visit : www.freekcsepastpapers.com

**UFAHAMU** **(Alama 15)**

1. **Soma makala yafuatayo kisha ujibu maswali**

Katika manifesto ya serikali ya Jubilee mwaka wa 2013, moja kati ya ahadi waliyopania kutimiza kwa ukamilifu ni elimu hasa ya msingi bila malipo. Hili lingewaauni wazazi wengi hasa kutoka maeneo ya mashambani wanaochuana na hali ngumu ya maisha kila uchao. Kupunguzwa kwa mzigo wa kulipa karo kungewasaidia wazazi kuwaelimisha watoto wao na kuimarisha ndoto yao ya maisha bora siku za halafu.

Hata hivyo, mpango huo adimu ulikumbwa na changamoto si haba. Furaha ya wazazi wengi iliyeyuka kama ua jangwani. Watoto wengi walishindwa kujiunga na shule kama ilivyokuwa imetarajiwa. Wengi waliishi kusononeka na kulalamikia changamoto ainati zilizodidimiza ufanisi wa mpango huo.

Idadi kubwa ya wanafunzi katika kila darasa inafanya utoaji wa elimu kuwa gumu. Kulingana na utafiti uliofanywa na wataalamu wa sekta ya elimu, darasa linastahili kuwa na wanafunzi kati ya ishirini hadi thelathini na watano. Hali hii itamwezesha mwalimu kukimu mahitaji ya wanafunzi hao kwa ukamilifu. Kinaya ni kuwa, katika shule nyingi nchini, idadi ya wanafunzi katika darasa ni kati ya themanini na mia moja hasa katika shule za msingi. Utoaji wa elimu katika hali hii umekuwa mgumu kwa sababu mwalimu analemewa kuwahudumia na hata kuwadhibiti wanafunzi darasani. Juhudi zingefanywa ili kupunguza idadi hii pengine kwa kujenga shule zaidi.

Ukosefu wa walimu wa kutosha shuleni pia ni mzigo katika kutimiza ndoto hii. Elimu bora hutegemea idadi ya walimu wanaotoa huduma hiyo. Kulingana na chama cha kupigania maslahi ya walimu nchini, taifa hili linahitaji zaidi ya walimu elfu mia moja ili kutoa elimu bora.

Ukosefu wa vifaa vya kutosha kama vile vitabu, madarasa na madaftari kwa kiasi kikubwa umeduwaza kusudio la mpango huu. wanafunzi wanahitaji vitabu vya kutosha darasani ili kudurusu ipasavyo. Hivi majuzi nilipigwa na butwaa kumsikia waziri wa elimu akisema kuwa serikali ina mpango wa kuteua kitabu kimoja kutumiwa na wanafunzi ili kupunguzia wazazi mzigo. Iwapo serikali inadai kutoa elimu bila malipo,ni mzigo huu utakaowalemea wazazi? Kwa maoni yangu hatua hii itadunisha kiwango cha elimu nchini. wanafunzi wanastahili kutafiti zaidi kuhusu masuala ya elimu. Hivyo wanahitaji maoni ya wasomi mbalimbali kama ilivyo katika vyuo vikuu.

Ufujaji wa pesa za elimu bila malipo unaotekelezwa na baadhi ya walimu na wasimamizi wa elimu nyanjani umechangia kudumaza elimu bila malipo. Nilimsikiliza Bwana Odinga alipokuwa akizindua manifesto ya NASA hapo jana, takribani siku arobaine kabla ya uchaguzi mkuu wa Agosti mwaka huu wa 2017. Lengo lake na lile lililotolewa na Rais Uhuru siku iliyotangulia huko Kasarani kuhusu elimu bila malipo, ni dhabiti. Hata hivyo matarajio yao yatategemea mikakati ya kudhibiti matumizi mabaya ya fedha zilizokusudiwa kuwaelimisha watoto wetu.

Natumai pia mipango itafanywa ili kudhibiti migomo ya mara kwa mara inayotatiza malengo ya serikali katika utoaji wa elimu. Walimu wanapogoma, taratibu za masomo huvurugwa. Wanafunzi kwa upande wao hasa was hule za upili, husukumwa na shinikilo rika na hata amatumidi ya mihadarati na kusababisha uharibifu wa mali hasa wanapoteketeza mabweni.

For free past papers visit: www.freekcsepastpapers.com

Maswali

1. Ipe taarifa hii anwani mwafaka (alama 1)

---

2. Mpango huu unewanufaisha vipi wazazi? Onyesha njia 4 (alama 4)

---

---

---

---

3. Idadi kubwa ya wanafunzi darasani ina athari gani? (alama 3)

---

---

4. Eleza changamoto zaidi zilizorejelewa. (alama 4)

---

---

---

---

5. Eleza maana ya maneno haya (alama 3)

   Pania
   
   ---
   
   Auni
   
   ---

for free past papers visit : www.freekcsepastpapers.com

Ufujaji

---

**Soma taarifa ifuatayo kisha ujibu maswali** **(alama 15)**

Utangamano ni hali ya watu kuishi pamoja bila kuzozana licha ya kuwa wanatoka katika makabila mbalimbali. Nchini Kenya kuna makabila takribani arobaini na mawili. Nchi ambayo ina makabila mengi hivi huwa na changamoto. Raia wengi hujikuta wakizozona kuhusu mambo fulani kwa sababu ya tofauti za kikabila. Wakati wa kuapishwa kwa rais wa nne nchini - Uhuru Kenyatta, alisisitiza kuwa nchi hii inafaa kuwa na utangamaano kwa sababu, uchaguzi si uadui. Rais alikuwa akilenga kuhimiza mtagusano na utangamano wa kitaifa. Nchi ambayo watu wanatangamana, huwa na ukwasi wa kiuchumi. Hii ni kwa sababu wananchi wanaweza kufanya biashara zao au kuendeleza shughuli zao bila utata au wasiwasi.

Wahenga walisema kuwa, umoja ni nguvu, utengano ni udhaifu. Juhudi za kuimarisha utangamano zinaweza kuafikiwa kupitia michezo. Wachezaji wanapojumuika uwanjani, daima hawajali kabila lao. Wao huzingatia kucheza kama timu. Fauka ya hayo,wao pia huzingatia ushindi katika mechi husika. Iwapo ni soka kwa mfano, utawapata wachezaji kutoka makabila tofauti. Mashabiki wanapojikusanya na kushabikia timu wazipendao, wao hufanya hivyo kama wakenya wala si kama kabila fulani. Bao likifungwa na mchezaji kutoka kabila la Kiluhya kwa mfano, mashabiki wote wa timu iliyofunga bao hushangilia. Utangamano wa kitaifa huweza kuhakikisha mazingira bora na utulivu katika jamii na hata nchi kwa ujumla.

Utagamano wa kitaifa pia unaweza kuimarishwa kupitia juhudi na viongozi wa dini. Waumini wanapokutana na kuabudu moja kwa moja kukutana huko ni njia moja ya kutangamanisha watu. Fauka ya hayo viongozi hao wanaweza kutumia nafasi zao na kuhubiri umoja katika jamii. Wanaweza kusisitiza kuwa wanadamu wote waliumbwa na Mungu mmoja na kwa hivyo wote ni sawa. Utangamano huu wa watu unaweza kusababisha nchi yote kuwa moja na kuhimiza yanayokaririwa katika wimbo wetu wa taifa, tukae na amani, upendo na umoja ili tupate raha na ustawi.

Matumizi ya lugha ya Kiswahili kama Lugha ya Taifa na Lugha Rasmi, kumechangia sana katika kukuza utangamano wa kitaifa. Watu kutoka makabila mbalimbali wanaweza kuwasiliana na kuwa kitu kimoja kutokana na matumizi ya lugha moja. Kulikuwa na muswada katika bunge lililomalika kuwa, katika ofisi za umma kusitumiwe lugha za kienyeji au za mama. Lugha ya Kiswahili inafaa kusisitizwa au ile ya Kiingereza ili kuimarisha mtagusano katika ofisi za umma. Licha ya kuwa muswada huo hukupitishwa, lilikuwa ni pendekezo ambalo lingeboresha umoja wa kitaifa na kuondoa dhana za kikabila katika ofisi za umma.

Tamasha za muziki au maigizo katika shule zetu za msingi na ipili, huchangia pakubwa katika kuimarisha umoja wa kitaifa. Wanafunzi kutoka sehemu zote za nchi wanapokongamana na wenzao, wanabadilishana maoni na kuimarisha urafiki kati yao. Urafiki huu unakuza utangamano wa kitaifa. Ni furaha iliyoje kuona wanafunzi kutoka Lodwar, Kisumu, Bungoma, Nyeri, na kwingineko katika jamhuri wakitangamana na kubadilishana mawazo kuhusu mambo yanayokumba jamii?

for free past papers visit: www.freekcsepastpapers.com

Shule za kitaifa nchini pia zimechangia kukuza utangamano huu. Ni jambo la kupendeza kuwapata wanafunzi kutoka sehemu mbalimbali kama vile Mandera, Kakuma, Kericho, Kitale, Migori, Mumias, na kwingineko, wamekutana katika shule za upili za kitaifa kama vile; Alliance, Mang'u, Starehe, Kamusinga, Lenana, Maseno, Kenya High, Loreto, Limuru, Utumishi, Pangani, Mary Hill na kusoma pamoja kwa muda wa miaka minne. Wanafunzi hawa hutangamana madarasani, maabadini, katika vyumba cha maakuli, nyugani, na kwingineko. Shule hizi za kitaifa basi zinatoa nafasi muhimu sana kutangamanisha wakenya.

for free past papers visit : www.freekcsepastpapers.com

**Swali**

Utangamano wa taifa unaweza kuboreshwa vipi? Jadili njia **kumi na tatu.** ( alama 15, maneno 90-100)

**Matayarisho**

**Jibu**

**Matumizi ya lugha** **(alama 40)**

a) (i) Taja na utofautishe sauti mwambatano za menoni. (ala 2)

---

(ii) Andika neno lenye mfumo ufuatao wa vitamkwa. Nazali ya ufizi + kipasuo cha kaakaa gumu + irabu ya juu nyuma + kizuiwa ghuna cha kaakaa laini + irabu ya chini wastani. (ala 2)

---

b) i) Eleza maana ya kiambishi kisha utoe mfano (ala 2)

---

---

ii) Tumia **ki**'katika sentensi kuonyesha hali ya kuendelea kwa kitendo kwa muda (ala1)

---

---

c) Onyesha muundo wa silabi katika neno wachanjwao (ala 2)

---

d) Ainisha maneno katika sentensi ifuatayo
Shehena ya dawa ilikuwa bandarini (al 1)

---

e) Tumia mzizi- enye katika sentensi kama kihusishi (ala1)

---

f) Sahihisha sentensi hii kwa namna mbili
Wasichana mabinti mapacha walipita mtihani. (ala 2)

---

---

for free past papers visit : www.freekcsepastpapers.com

g) Ainisha virai katika sentensi ifuatayo.
Amenijibu kwa hasira (ala2)

---

---

h) Unda nomino moja kutokana na nomino zozote mbili za Kiswahili (al1)

---

i) Changanua sentensi ifuatayo kwa kielelezo cha jedwali:
Ule mkongojo ulioletewa babu utauzwa na fundi maarufu. (al 3)

j) Kamilisha sentensi ifuatayo kwa kielezi cha namna kugizi. (al 1)
Sauti ya mtoto haikusikika ilikuwa imedidimia ------------ mama alipofika

---

k) Andika visawe viwili vya nahau, **fanya inda** (ala 1)

---

l) Tunga sentensi mbili tofauti kudhihirisha kuwa neno **bunda** ni kitawe.
(ala 2)

m)
(i) Akifisha sentensi ifuatayo kuonyesha usemi halisi: (ala1)
Mama atakuja kesho

---

n) Changanua vipashio vya kisarufi katika kiarifa cha sentensi ifuatayo.
Hawa ndio waliopigana (ala 2)

---

o) Nomino zifuatazo zimo katika ngeli gani? (ala 1)
(i) Siwa (ii) Kipunye

---

for free past papers visit : www.freekcsepastpapers.com

p) Andika sentensi ifuatayo upya ukitumia neno badala ya -ki ya masharti. (ala1)
Ukifika mapema utampata.

---

q) Bainisha viwakilishi nafsi katika sentensi ifuatayo:

Mimi ninataka kumwona mwanariadha aliyepata nishani ya dhahabu (ala 2)

---

r) Eleza maana mbili za sentensi:
Mama atawaalika wengine. (ala 2)

---

s) Geuza sentensi ifuatayo katika kauli ya kutendata:
Miyaa maridadi ilisukwa na msusi stadi. (ala 2)

---

t) Kanusha sentensi ifuatayo katika hali ya mazoea. (ala1)
Amekuja hapa

---

(ii) Andika kwa msemo halisi: (ala 2)
u) Tajiri alishangaa kuwa niliweza kuubeba mzigo huo peke yangu.

---

v) Andika sentensi ifuatayo upya kwa kufuata maagizo. (ala1)
Mama anapika kutwa kwa sababu ya wageni (Tilia mkazo kwa kinyume)

---

x) Tunga sentensi na ubainishe namna mbili za uamilifu wa kundi nomino (ala2)

---

---

y) Andika methali **nne** zinayoafiki maelezo:
Hakuna chema kisichokuwa na madhara. (ala 4)

for free past papers visit : www.freekcsepastpapers.com

---

---

---

**4. Isimujamii** **(alama 10)**

a) Eleza sababu **nne** zinazowafanya vijana kupenda kutumia sheng' katika mawasiliano yao. (alama 4)

---

---

---

---

b) Fafanua jinsi mambo hafuatayo huweza kusababisha kutoweka kwa lugha: (alama 4)

i) Vita

---

---

ii) Ndoa za mseto

---

---

c) Huku ukitoa mifano, bainisha mbinu mbili zinazotumiwa kuunda istilahi mpya katika jamii ya leo (alama2)

---

---

---

for free past papers visit : www.freekcsepastpapers.com